

Sina Habari Mwanangu

Sina habari, mwanangu
sina habari
Isipokuwa
habari ya taabu, mateso, na kifo.

Sina habari, mwananchi
sina habari.
Ukitaka aardhi, ukitaka chakula
sina habari
Isipokuwa
habari za risasi na vita.

Sina habari, mzalendo
sina habari
ukitaka shamba, ukitaka haki
nyumnba na nguo
sina habari
Isipokuwa
habari ya mapambano

Sina habari, mwanangu
sina habari.
Ukitaka maisha
Lazima uwetayari
kupambana
kupambana tena.

Sina habari, mwanangu sina habari
Isipokuwa
habari za taabu, mateso, na kifo.

Eh, mwanangu,
ukotayari
kusikia habari?

Shiraz Durrani
[February 15, 1985]